

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO



TANGAZO

TUZO YA SAMIA KWA VIJANA KATIKA KILIMO

WITO WA KUWASILISHA ANDIKO LA WAZO BUNIFU LA MRADI WA KILIMO KWA VIJANA WALIOPO VYUONI

Wizara ya Kilimo inapenda kuwakaribisha vijana wa Kitanzania kuandaa na kuwasilisha wazo la mradi utakaoleta mabadiliko katika Sekta ya Kilimo kwa maendeleo ya uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Wazo hilo la mradi lilenge kwenye kutatua changamoto za sekta ya kilimo kwenye maeneo yafuatayo: Tija na uzalishaji mdogo; matumizi madogo ya pembejeo za kilimo kama mbegu, mbolea, viuatilifu na zana za kilimo; upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno; huduma hafifu za ugani katika kilimo, ushiriki mdogo wa vijana na wanawake katika kilimo; ukosefu wa masoko na ugharamiaji wa sekta ya kilimo.

Miradi mitatu bora itachaguliwa na kupatiwa msaada wa kifedha na kitaalamu ili kufanikisha utekelezaji wake.

Vigezo vya kushiriki:

- i. Awe Mtanzania
- ii. Awe kijana mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
- iii. Awe ni mwanafunzi katika Vyuo vya Kati au Vyuo Vikuu

Mambo ya kuzingatia katika andiko linaloandaliwa:

- i. Andiko la Mradi lisizidi maneno 3,000.
- ii. Andiko lieleze mradi utakavyochangia malengo ya kitaifa katika Sekta ya kilimo.
- iii. Andiko liwe rahisi kusomeka kwa kutumia ukubwa wa maneno (font size 12), aina ya maneno (Arial) na nafasi kati ya mstari iwe 1.5.
- iv. Andiko liandaliwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza
- v. Andiko liainishe idadi ya watekelezaji wa mradi na weledi wao
- vi. Andiko lieleze jinsi mradi utakavyosaidia kutoa ajira kwa vijana wengine na matokeo yake kuwa endelevu.
- vii. Barua (Covering Letter) ya kuwasilisha Andiko la wazo bunifu iambatishwe na wasifu (Curriculum Vitae) wa Mwandishi wa Mradi
- viii. Andiko liwe pamoja na bao la Mantiki (project logframe) linaloonesha malengo/madhumuni ya mradi, viashiria vya utendaji (performance indicators), matokeo tarajiwa kutoka kwenye mradi na shughuli za mradi.
- ix. Andiko liwasilishwe kwa barua pepe competition@kilimo.go.tz kuanzia tarehe 15 hadi 29 Februari 2024 kabla ya saa 6.00 Usiku.

Motisha kwa Washiriki

- i. Mshindi wa kwanza atapata kiasi cha Shilingi Milioni tano (5,000,000/=)
- ii. Mshindi wa pili atapata kiasi cha Shilingi Milioni nne (4,000,000/=)
- iii. Mshindi wa tatu atapata kiasi cha Shilingi Milioni tatu (3,000,000/=)
- iv. Mshindi wa nne atapata kiasi cha Shilingi Milioni mbili (2,000,000/=)
- v. Mshindi wa tano atapata kiasi cha Shilingi Milioni moja (1,000,000/=)
- vi. Mshindi wa sita hadi wa kumi (6-10) watapata kiasi cha Shilingi Laki Tano (500,000/=) kila mmoja.

Vijana na Wanawake wanahamasishwa kuwasilisha maombi ili kuwa sehemu ya mageuzi katika Sekta ya Kilimo.

Imetolewa na:



**KAIMU KATIBU MKUU
WIZARA YA KILIMO**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF AGRICULTURE



ANNOUNCEMENT

SAMIA AGRICULTURE YOUTH AWARDS

**CALL FOR SUBMISSION OF AN AGRICULTURE INNOVATIVE IDEAS FOR
YOUTH IN COLLEGES**

The Ministry of Agriculture would like to announce to Tanzanian youth to prepare and present an innovative idea for a project that will bring transformation in the Agriculture Sector for the social economic development and the Nation as a whole. Your innovation idea should focus on addressing agricultural sector challenges which include: low productivity and production, inadequate use of agricultural inputs, crop post-harvest losses, inadequate extension services, low involvement of youth and women in agriculture, and inadequate access to market and agriculture financing.

The best three projects will be selected and given financial and technical support.

Participation criteria:

- i. Be a Tanzanian
- ii. Age between 18 and above
- iii. Nominees must be student in College or University

Project Document requirement:

- i. The document must not exceed 3,000 words
- ii. The project must contribute to national goals in the agricultural sector
- iii. Explain how the project will help to employ other youth
- iv. The document should be easy to read using font size -12, type of words -Arial, and the space between lines should be 1.5
- v. The document should be prepared in English or Swahili language
- vi. The applicant should specify the number of project implementers and their expertise to demonstrate the ability to implement the project, and its outcome to be sustainable
- vii. Covering Letter to submit innovative project be attached with curriculum vitae
- viii. Must submit Project Log Frame showing the goals/objectives of the project, performance indicators, project activities, and expected results from the project, and

- ix. Submit your project document through email: competition@kilimo.go.tz from **15th to 29th February 2024 before 12:00 PM.**

Incentives for Participants:

- i. The first winner will receive five million Tanzanian Shillings (5,000,000/=)
- ii. The second winner will receive four million Tanzanian Shillings (4,000,000/=)
- iii. The third winner will receive three million Tanzanian Shillings (3,000,000/=)
- iv. The fourth winner will receive two million Tanzanian Shillings (2,000,000/=)
- v. The fifth winner will receive one million Tanzanian Shillings (1,000,000/=)
- vi. The sixth to tenth (6-10) winners will receive five hundred Shillings (500,000/=) each.

Youth and Women are encouraged to apply.

Issued by:



**ACTING PERMANENT SECRETARY
MINISTRY OF AGRICULTURE**